

Usimulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*

Rosemary N. Burundi, Mwenda Mukuthuria
na
Enock S. Matundura

Ikisiri

Makala haya yanachunguza usimulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* uliotungwa na Hassan bin Ismail. Yanachunguza jinsi fani ya usimulizi, iliyodaiwa na wahakiki wa ushairi wa Kiswahili kuupa utenzi huu upekee, ilivyotumiwa na mtunzi ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe husika. Mambo ambayo tumedhamiria kuyachunguza ni yale yanayohusiana na usimulizi kama vile maudhui (yanayosimuliwa), msimulizi, aina za usimulizi, na maajenti wa usimulizi. Makala haya yana sehemu tatu; sehemu ya kwanza ni utangulizi unaofafanua usuli wa mada ya utafiti na madhumuni ya utafiti, sehemu ya pili inaonesha nadharia iliyoongoza utafiti na sehemu ya tatu ni matokeo ya utafiti na hitimisho. Huu ni utafiti wa kifasihi ambao umefanyiwa maktabani kwa kusoma, kuchambua na kuhakiki matini ya utenzi na kuwasilisha matokeo ya uchunguzi.

1.0 Utangulizi

Utenzi wa Swifa ya Nguvumali ulitungwa na Hassan bin Ismail aliyezaliwa Kilwa mjini kama inavyodhihirika katika Lienhardt (1968: ubeti 393). Alipata kariha ya kuutunga baada ya kupokezwa kitabu na mamake kutoka kwa babuye (mtunzi) aliyekuwa mtunzi zamani kama inavyobainika katika beti za 385- 389. Kwa mujibu wa Liendhardt (1968) utenzi huu ulikuwa ukikaririwa kutumbuiza watu katika hafla mbalimbali kabla haujawekwa katika maandishi kutoka imla ya mtunzi iliyochukua karibu siku tatu. Kwa hivyo, kama ilivyodokezwa na watafiti katika ushairi wa Kiswahili, ulikuwa katika hali ya masimulizi kabla ya kuandikwa (Knappert, 1979). Umetungwa katika lahaja ya Kimrima inayozungumzwa kusini mwa Tanzania hasa kuzunguka eneo la Kilwa (Gerald, 1981; Mukuthuria, 2007). Hata hivyo, mtunzi ameonesha athari ya lugha ya Kiarabu kama ilivyo katika mashairi ya zamani. Aidha, ameathiriwa na lahaja za kaskazini kama vile Kiamu na Kimvita zilizokuwa na historia ndefu ya utunzi wa mashairi. Jambo jingine linalobainika wazi na linaloutofautisha utenzi huu na tenzi sifika kama vile *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Hamziyya*, *Utenzi wa Al-Inkishafi*, *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mwanakupona* ni kuwa mtunzi ametohoa maneno mengi ya Kiingereza. Athari hii ya lugha ya Kiingereza inaakisi muktadha wa kihistoria ambapo ukoloni wa Kimagharibi ulikuwa umekita katika mwambao wa Afrika ya Mashariki, utenzi huu ulipotungwa. Tenzi hizo nyingine hazijaonesha athari ya Kiingereza kwa

kuwa zilipotungwa Waingereza hawakuwa wameingia sehemu hizi. Kwa mujibu wa Liendhardt (1968) na Gerald (1981), utenzi huu uliwekwa katika maandishi miaka ya 1950. Wakati huu Waingereza walikuwa wakitamalaki janibu hizi za Afrika ya Mashariki na lugha yao kutumiwa hata kufundishia (Chiraghdin na Mnyampala, 1977).

Japo utenzi huu haukutungwa katika karne ya 18, kama tenzi nyingine sifika miongoni mwa jamii ya Waswahili, kwa maoni yetu ni kazi ya sanaa inayostahili heshima na sifa zinazopewa tenzi hizi na pia kutafitiwa. Umesifiwa kuwa bulibuli na wahakiki wa ushairi wa Kiswahili. Mukuthuria (2007) ameubainisha kama 'Utenzi wa Mpito, Mseto wa Imani za Jadi na Usasa.' Kwa hivyo, maudhui ambayo hayajapitwa na wakati ni suala linalouweka katika kiwango cha upekee. Suala jingine analodai limeupa upekee ni usanii unaobainika katika matumizi ya fani ya usimulizi. Kutokana na kauli hii, utafiti huu ulilenga kuchunguza ni kwa jinsi gani fani ya usimulizi imefanikishwa na mtunzi katika kudhihirisha na kuyaendeleza maudhui yake.

Ilibainika kuwa tangu utenzi huu ulipowekwa katika maandishi katika awamu ya kwanza ya karne ya 20, haujavutia machapisho mengi ya tahakiki kutoka kwa wataalamu wa fasihi ya Kiswahili ukilinganishwa na tenzi nyingine bulibuli. Aidha, tafiti nyingi zilizofanywa, pamoja na tahakiki katika fasihi ya Kiswahili zimeelemea upande wa maudhui (Mohochi, 2000). Katika utanzu wa ushairi, hasa tenzi, tuna tafiti kama vile za Gibbe (1994), Momanyi (1998) na Masinde (2002) ambazo zimeshughulikia maudhui. Imebainika kuwa ni tafiti chache tu zinaangazia usanifu wa kuyawasilisha maudhui (Momanyi, 1991; Karama 1996; Nyanchama, 2004). Mohochi (2000) anasisitiza kuwa uendelezaji wa fasihi hasa kwa upande wa uhakiki na utafiti unapaswa kuzingatia pande zote mbili, yaani maudhui na fani. Kutokana na hali hii utafiti huu umezingatia kipengele cha usimulizi ambacho ni cha kifani ili kuziba pengo hili. Kwa ujumla, ulidhamiria kuchunguza yaliyosimuliwa na mikabala ya usimulizi iliyotumiwa kufanikisha vitushi vya *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*.

2.0 Maoni ya Wataalamu kuhusu Fani ya Usimulizi

Suala la usimulizi limetafitiwa na kushughulikiwa na wataalamu mbalimbali hasa katika uandishi au usimuliaji wa hadithi na wametoa maelezo kadha wa kadha ambayo ni muhimu katika utafiti huu. Kanar (2001) amesema kuwa usimulizi ni mtindo wa mpangilio unaotumiwa na waandishi wa hotuba, habari na utunzi wa kibunilizi kueleza matukio. Anaendelea kufafanua kuwa unahusisha hadithi inayosimuliwa na msimulizi. Kulingana na mtaalamu huyu, kuna kaida maalumu ambazo sharti msimuliaji azitilie maanani wakati wa kutoa masimulizi yake kwa kuwa hadhira yake huzitarajia, na huwa wanazisaka wanaposoma au kusikiliza kisa. Nazo ni:

- a) Ni kina nani wanaohusika? (watendaji)
- b) Ni nini kinatukia? (matukio)
- c) Ni lini yanatukia? (wakati)
- d) Kwa nini yanatukia? (msukumo)

Mawazo ya mtaalamu huyu yanalandana na ya Baldick (1990) anayeeleza usimulizi kama mfanyiko unaohusisha utoaji wa matukio kwa mpangilio wa kufuatana. Kulingana naye, mtindo wa usimulizi unaweza kulinganuliwa na uelezaji au usemezano ambao huwa ni mitindo mingine inayoweza kupatikana katika masimulizi.

Wakishughulikia kigezo cha usimulizi katika riwaya, Mazrui na Syambo (1992) wamebainisha aina nne za usimulizi. Mojawapo ni usimulizi wa mwandishi mwenyewe akitumia viambishi vya nafsi ya tatu. Kwa maoni yao, usimulizi huu unamwezesha mtunzi kusimulia matukio yote pamoja na matokeo yake popote. Anaweza kuingia bongoni na nyoyoni mwa wahusika na kueleza mawazo na hata hisia. Pili, ni usimulizi wa mmoja wa wahusika akitumia nafsi ya tatu. Katika kufafanua usimulizi huu, wameeleza kuwa msimulizi huyu hueleza mawazo, hisia na vitendo vya wahusika wengine. Tatu, ni usimulizi wa mwandishi akitumia viambishi vya nafsi ya tatu, lakini tofauti na aina ya kwanza, huwa haelezi yale ambayo hayakujidhihirisha katika maneno au vitendo vya wahusika. Kwa hivyo, si mjuzi wa mawazo na hisia za wahusika. Kwa maoni yao, riwaya inayotumia usimulizi wa namna hii huwa na mazungumzo mengi ambayo kwayo fikra na mawazo hudhihirika. Msomaji huachiwa jukumu la kung'amua bila kuelezwa sababu za vitendo na maneno ya wahusika. Nne, ni usimulizi wa mmoja wa wahusika akitumia viambishi vya nafsi ya kwanza. Kwa maoni ya wataalamu hawa usimulizi huu humfanya mwandishi na msimulizi kuwa kitu kimoja na msomaji. Huwa wamekaribiana zaidi kwa kuwa mhusika-msimulizi husema nao moja kwa moja bila ya maelezo ya kupitia kwa mwingine. Kimsingi, kazi hii ya wataalamu hawa imetusaidia kuchunguza anayesimulia kisa katika matini ya *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Imetufahamisha kuwa mtunzi wa kazi ya kifasihi huchagua njia ya kusimulia itakayomwezesha kulifikia lengo lake barabara.

Msimulizi ni wakala au nyenzo inayotumiwa na mtunzi kusimulia hadithi. Kwa hivyo, kila hadithi ina msimulizi ambaye anaweza kuwa mtunzi au mtu mwingine ambaye amemteua awe msimulizi. Hadithi inamfikia msomaji kupitia kwa msimulizi. Msimulizi humpitisha msomaji au msikilizaji katika masafa, maeneo, nyakati na katika mawasiliano ya wahusika, hali na saikolojia zao. Kwa hivyo, msimulizi kupitia usimuliaji anajenga mkabala ambao unamwezesha msomaji au mtazamaji kuyatazama yanayotendeka na kuyasikia yanayosimuliwa. Kama ambavyo wataalamu wa fasihi wameeleza, kuna njia nyingi za kusimulia ambazo mtunzi au msimulizi anaweza

kutumia kuwasilisha kisa chake (Msokile, 1993; Mohamed, 1995; Mohochi, 2000; Mbatia, 2001; Wamitila, 2003). Njia hizi humwongoza msomaji kwa kile kinachosimuliwa huku nyingine zikiashiria msimamo, maoni, mwelekeo au hata mapendekezo yake mtunzi. Kuhusu msimulizi, wataalamu wa fasihi wameeleza kwamba anaweza akawa wa nafsi ya kwanza, pili au tatu. Aidha, anaweza kuwa mshuhudaji wa matukio au mshiriki katika matukio anayoyasimulia. Pia, anaweza kujitokeza bayana na kujitambulisha au hajitokezi bayana (Mazrui na Syambo, 1992)

3.0 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Usimulizi/Naratolojia. Kwa mujibu wa Wamitila (2002, 2003), nadharia hii iliwekewa misingi ya mwanzo na mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato, katika maandishi yake ya *The Republic III* yaliyoandikwa miaka 360 kabla ya kuzaliwa Kristo. Nadharia hii inahusika na uchunguzi wa hali, muundo na uamilifu wa hadithi na kubainisha umilisi wa kisimulizi alionao mtunzi. Aidha, huchunguza sifa zinazohusisha simulizi na kuzitenganisha nyingine. Wamitila anaeleza kuwa mawazo haya ya Plato yamefumbatwa kwa dhana mbili za kimsingi, ambazo ni *Mimesia* na *daigesia*. Katika *Mimesia* mtunzi hajitokezi wazi; huwa amefichika ilhali katika *daigesia* anajitokeza waziwazi kama msemaji na anatambulika. Mwanafunzi wa Plato, Aristotle (katika kazi yake “Poetics” – taf. S.H. Butcher, 1994 -2009) alipanua maana ya dhana ya *mimesia* kwa kuihusisha na kueleza. Kulingana naye, kipengele cha kueleza kina sifa ya *ki-mimesia*.

Masuala muhimu katika Nadharia ya Naratolojia ni kwamba uchunguzi wa kinaratolojia unatambua na kukubali kuwa simulizi au hadithi hutambwa kwa njia mbalimbali kama vile ya nathari au kishairi, andishi au simulizi; kuwa matukio katika matini yoyote huweza kuwasilishwa kwa jinsi mbalimbali. Jinsi kuu ni uelezaji na uoneshaji au katika kutumia istilahi za ki-Plato, yaani *mimesia* na *daigesia*. Kuwa, matukio yoyote yale hutendeka wakati maalumu. Uhakiki wa kinaratolojia hubainisha kati ya Wakati-Matini na Wakati- Hadithi. Suala jingine linalowajuzu wana-naratolojia ni wakala wa usimuliaji. Kipengele kingine kinachowashughulisha ni mkabala wa kimtazamo. Msimulizi au mwandishi wa hadithi huwa na mtazamo kuhusu masuala kadhaa ambayo hutaka kushirikisha hadhira. Kwa hiyo, kwa kutumia nadharia hii tutaweza kuchambua vizuri utenzi husika.

4.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Kazi mbalimbali za kifasihi na hasa zilizozingatia utafiti wa ushairi zilipewa kipaumbele. Utenzi uliolengwa, *Utenzi wa Swifa ya*

Nguvumali, ulisomwa kwa kina, ukahakikiwa kupitia uchanganuzi wa kithamano, ambapo maelezo hutathminiwa kumwezesha mtafiti kutoa maoni ya kiujumla.

5.0 Yaliyosimuliwa katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*

Mtunzi wa utenzi huu amesimulia kisa ambapo wachawi wanne; Bwana Shambi bin Dima, Binti Jizi, Binti Ramadhani na Binti Hanifu wanakutana kwa siri jioni moja na kumtaka mmoja wao kumtoa ndugu yake mhanga ili wamtoe sadaka kuuzingua mji wao, kama inavyodokezwa katika beti zifuatazo:

10.	Wachawi wanne yaqini	16.	‘Sikilizeni nisemayo
	Walikutana jioni		Tena mukae kituo
	Shauli gani jamani		Tufanye mji zinguo
	La kuweza kutumia?		Miaka imetimia.

Wote wanaafikiana kwamba ilikuwa zamu ya Binti Hanifu kutoa kafara. Wanamsisitizia kwamba anayetakiwa ni nduguye, mtoto wake au hata yeye mwenyewe, lakini si jirani yake (ubeti wa 19, 23). Baada ya maafikiano yao, wanafunga Mwezi mtukufu wa Ramadhani. Baadaye kinara wao, Bwana Shambi anamtuma Binti Jizi kwenda kuwaita wenzake ili wakutane mahali pao pa siri ili watekeleze njama yao bila kuchelewa (ubeti 46). Binti Jizi anawakuta wenzake wakiwa na shaka na hofu kuu baada ya kupata njozi zinazoashiria kutokea kwa mkosi, kama inavyobainika katika (beti 49-50).

Hata hivyo, Binti Jizi anafaulu kuwashawishi kwamba hawana budi kutekeleza njama yao na kuwa hawawezi kumvunja kinara wao. Binti Jizi anawaeleza (beti 51-57) kufanya hivyo ni sawa na kujitakia mabaya. Wanakubaliana kukutana kama walivyokuwa wameafikiana lakini mmoja wao Binti Ramadhani ambaye ni mama mkwe wa Binti Hanifu, hakufika kama walivyokubaliana. Alibaki nyumbani akijidai anaumwa (beti 60-62). Kinara wao Bwana Shambi anamshurutisha Binti Ramadhani kujiunga na wengine (beti 63-64). Anaenda huku akimwacha mkaza mwana Salima nyumbani.

Mtunzi anazidi kusimulia (beti 68-79) kuwa Salima alivutwa kwa urogi na kwenda mpaka msituni ambapo wachawi hawa walikuwa wakimngojea bila kujifahamu. Anapofika huko msituni, dadake Binti Hanifu anamnyanyua na kumkabidhi kwa wachawi wenzake ili kulipa deni lake kwao. Wanamchukua na kumpaka dawa za kumpumbaza (ubeti 86) kisha wanamfunga kwenye mti na kumwacha hapo (ubeti 95). Wanarudi kijijini na kukuta habari za kupotea kwake zikiwa zimetanda. Wanaungana na wengine katika harakati za kumtafuta huku wakisubiri usiku kuingia ili waendeleo kutekeleza mpango wao. Msimulizi anatupeleka tena msituni ambapo wachawi wanarudi

kumchukua Salima. Kinyume na walivyotarajia wanakuta hali yake si hoi; aliweza kuwatambua na akajibizana nao hasa kumlaani dadake Binti Hanifu kwa kumtendea unyama huo (ubeti 110). Mmoja kati ya wachawi hao, Binti Ramadhani anahuzunishwa na kilio cha Salima na kuwarai wenzake wamrudishe nyumbani kama alivyotaka (ubeti 122). Hata hivyo, kinara wao Bwana Shambi alikataa kwa kuwaeleza kwamba kufanya hivyo itakuwa balaa zaidi kwao kwani hawana dawa ya kumlisha ili asiwaeleze wengine kijijini juu ya njama hii (ubeti 127). Binti Ramadhani anajiondoa kilingeni kwa majuto mengi na kuapa kuwa tangu siku hiyo hatakuwa mmoja wao (beti 129-132). Wachawi wanabaki watatu. Msimulizi anaendelea kueleza kuwa watu wengi walifika nyumbani kwa Salima na msako mkali ukafanywa. Juhudi zao ziliposhindwa kufua dafu, wazo la kutoa ripoti kwa serikali linazuliwa. Bwana Mwenye anajitoa kwenda mara moja bila kukawia ili kuepusha kijiji kutokana na adhabu. Anasema:

138. ‘Bassi sasa naondoka

Lipoti naipeleka

Isituwee mashakka

Halafu tukazangaa.

Lakini Binti Ramadhani anamshauri (beti 139-140) asubiri mpaka siku inayofuata. Hata hivyo, Bwana Mwenye hakusubiri. Alasiri ya siku hiyo alifika Ruvuja na kutoa habari.

Jumbe na Liwali wanapowasili Panenene, mkutano unaitishwa na msako unafanywa. Wanaposhindwa kufaulu Jumbe anataka ushauri kutoka kwa watu. Hapa ndipo Bwana Shambi (beti 184-185) anazua pendekezo kuwa mganga maarufu, Nguvumali, aitwe ili asaidie. Katika juhudi za kuficha siri ya njama yao isigunduliwe, Bwana Shambi anaamua kukutana na wazee 12 wa vijiji (ubeti 193). Wanakubaliana kuwa barua iandikwe kumwalika Nguvumali. Bwana Shambi anajitolea kwenda Ruvuja mbele ya wakili wake Bwana Kagendu kuidhinisha barua hiyo. Aidha, alikuwa tayari kugharimia shughuli hiyo (beti 190 -197). Baada ya hapo mtunzi anatueleza kuwa vijana wawili, Yasini Kimina na Hamadi Ramadhani (beti 200-207) wanatumwa kumpelekea Nguvumali waraka. Bwana Shambi anaporejea kwake kutoka Ruvuja, aliona nyoka wawili wakifuata kivuli chake na alipokaribia nyumbani kwake wakatoweka. Usiku uliofuata, anaota akibebwa kwa machela baada ya kuanguka. Pia, ndotoni anamwona Nguvumali (beti 219-224). Hali hii inamtia wasiwasi na anaamua kwenda msituni kuichukua maiti ya Salima na kuiweka katika kibanda kilichokuwa kimeanguka hapo kijijini. Aidha, anapanga na mchawi mwenzake Binti Hanifu kwamba atajifanya kuwa ameigundua maiti na kupiga yowe litakalowanabaisha watu wakimbilie huko (beti 232-237). Lakini kama mtunzi anavyotueleza, watu wanapoiona maiti wanaingiwa na shaka

kwa kuwa walikuwa wamefanya msako kila pahali. Ilikuwa wazi kuwa ile maiti ililetwa pale. Aidha, wanagundua kuwa ulimi wa maiti ulikuwa umekatwa na ndipo uamuzi wa kuwaita wawakilishi wa serikali - Liwali na Jumbe unaafikiwa ili kufanya uchunguzi kwa kuwa ilikuwa wazi uhalifu umetendeka (beti 238-260). Wanakijiji walikesha pale wakingoja polisi kufika kufanya uchunguzi. Msimulizi anatumia kwamba walipowasili waliendesha uchunguzi wao kwa fujo kubwa. Walikuwa wawili tu lakini walifanya vituko kwa kuwapiga watu makofi na mateke, ikawa ni kama walikuwa polisi 12 (beti 275-292). Kijiji chote kilisikitika kwa madhila ya hawa polisi. Polisi hawa wanarejelewa kama 'Mjaluo' na 'Mnyamwezi' (ubeti 284). Kwa mujibu wa Lienhardt (1968) makabila haya katika sehemu hii yalifahamika kwa ukatili wao.

Binti Ramadhani aliyekuwa amejitenga na wachawi wenzake, alitoa habari zilizosababisha kukamatwa kwa washukiwa (beti 286-289). Wakati huu wote, uchunguzi unapofanywa na polisi, Nguvumali alikuwa hajafika. Alipofika, Liwali aliandika barua kwa polisi akiomba washukiwa waachiliwe ili washughulikiwe na mganga Nguvumali (beti 298-300). Watu wengi wanakutanika kutoka sehemu mbalimbali kushuhudia kisa hiki. Nguvumali anajitayarisha kufanya kazi yake pamoja na wanafunzi wake (beti 317-319). Anawanyweshwa washukiwa dawa iliyokuwa na uwezo wa kuchagua na kuwaathiri tu wale waliohusika katika kitendo kibaya cha kuua, kama inavyobainika katika (beti 325 - 326):

325. Kilevi kilisitawi	326. Kinafata wale wale
Kwa wale wale wachawi	Waliyekuwa siku ile
Na wengine wasiwe	Waliyeua mtu yule
Sababu kinateua.	Ndio waliolewa.

Kama alivyokuwa ameota Bwana Shambi, aliathiriwa asiweze kusimama; ikabidi achukuliwe kwa machela na majirani na kupelekwa mpaka nyumbani kwake ambapo alitoa zana za kichawi. Wanawake wenzake pia, waliathiriwa na kileo walichopewa na Nguvumali na kukiri hadharani kushiriki mauaji japo hawakutoa vyombo vya kichawi kama kinara wao Bwana Shambi (ubeti 336). Ilikuwa wazi walihusika katika mauaji ya Salima. Nguvumali akawanyweshwa dawa ya kuondoa kileo kilichowafanya kueleza yote waliyokuwa wamefanya. Maelezo haya yakatumia kama ushahidi na akawakabidhi kwa Serikali ili hatua za kisheria zichukuliwe (beti 350-352). Walikuwa watatu baada ya mmoja wao Binti Ramadhani kufariki kama inavyobainika katika ubeti wa 338. Bwana Shambi alihukumiwa kifungo cha miezi tisa huku Binti Jizi na Binti Hanifu wakifungwa miezi mitano kila mmoja (ubeti 378). Walishtakiwa kwa makosa ya mauaji. Bwana

Shambi alijaribu kujitetea lakini kwa kuwa alikuwa ameshaungama makosa utetezi wake haukumfaa (beti 370-372).

Baada ya wachawi kufungwa, Nguvumali anapewa kibali na Serikali kuutumia uganga wake kuusafisha mji wa Panenene pamoja na miji mingine iliyokuwa karibu dhidi ya uchawi. Watu wote, katika miji kama Siwa, Mtambwe na Kunazini walilazimishwa kunywa dawa za Nguvumali. Aidha, walitozwa ada ya senti sitini kila mmoja (beti 360-365). Msimulizi anamalizia kwa kutueleza hatima ya Nguvumali mganga maarufu ambaye alifariki katika ajali ya barabarani (ubeti 382). Kama ilivyo kawaida katika usimulizi wa tenzi nyingi, mtunzi anajitambulisha (ubeti 389), kama Hassan Bin Ismail aliyezaliwa Kilwa Kivinje.

Katika kutamatisha hadithi iliyosimuliwa katika utenzi huu, mambo kadha yameangaziwa: mosi ni kuwa jamii iliyoshughulikiwa ina imani katika ushirikina, uchawi na uganga. Uchawi umedhihirishwa kama tendo la siri (ubeti 10) na lisilo na faida katika jamii japo wachawi hujifanya kuwa wanasaidia jamii (ubeti 16). Kwa upande mwingine sanaa ya uganga imebainika kama iliyoheshimiwa hasa kwa kuwa ilitumiwa kuwahudumia waliokuwa wameathiriwa na mikasa ya kichawi. Nguvumali anaitwa kusaidia kutatua shida iliyotukia katika jamii. Ana uwezo usiokuwa wa kawaida wa kuwatambua na hata kuwafanya wachawi kutoa zana za kichawi walizokuwa wakitumia. Miongoni mwa zana hizi ulikuwa ulimi uliokuwa mweusi kama lami. Aidha, walikiri kuhusika katika mauaji ya Salima (ubeti 334).

6.0 Msimulizi na Aina za Usimulizi katika Utenzi wa Swifa ya Nguvumali

Uchunguzi ulibainisha kwamba *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* umesimuliwa kwa kuzingatia mitindo miwili mikuu ya kisimulizi: usimulizi wa nafsi ya kwanza na usimulizi wa nafsi ya tatu. Kwa hivyo, usimulizi katika utenzi huu ni changamani. Usimulizi wa nafsi ya kwanza unabainishwa na matumizi ya mofu {na} na {ni} kwa mfano, mtunzi anaanza kwa kusema:

1. Bismilahi na anza Jina la mola wa enza Muhammadi mpendeza Kwa Mola wetu jalia.	2. Naku omba ya Rabbana Uni jalie kijana Ni tungapo shairina Pasiwe hudhia.
3. Rabbi ni pe fahamu Uni jalie elimu Na taka kuyahukumu Shairini kuyatia.	4. Nay atia shairini: Panenene na Kojani Mteniyapa mjini Khabari zilitokea.

Msimulizi ambaye amejibainisha katika beti hizi kama mtunzi amejitambulisha kwa kutumia viambishi viwakilishi ‘ni’ na ‘na’ ambavyo ni vya nafsi ya kwanza, wakati uliopo. Katika sehemu hii ambayo ni utangulizi, msimulizi (ambaye pia ndiye mtunzi) ameanza usimulizi kwa sala au maombi ambao ni mtindo wa kawaida wa kutanguliza tenzi (Allen, 1971; Knappert, 1979). Aidha, amebainisha kuwa anayoyasimulia aliyashuhudia. Ameeleza pale yalipotukia; kijiji cha Panenene na Kojani mji wa Mteniyapa. Usimulizi huu wa nafsi ya kwanza unaojitokeza katika beti za (1-9) unamfanya msomaji au msikilizaji kuwa na uhusiano wa karibu na msimulizi ambaye amejibainisha kama mtunzi. Anawasiliana moja kwa moja na msomaji wake. Aidha, anasimulia mambo ambayo aliyashuhudia yakitendeka.

Usimulizi huu wa nafsi ya kwanza unabadilika katika ubeti wa 10 ambapo msimulizi-mtunzi anaanza kusimulia matukio ambayo hakushiriki. Anaeleza walivyofanya watu wengine, kwa hivyo, mofimu {a} na {wa} na ‘yeye’ za usimulizi wa nafsi ya tatu zinautambulisha mkabala huu wa usimulizi kama inavyobainika katika beti zifuatazo:

10. Wachawi wane yaqini
Walikutana jioni:
‘Shauli gani jamani
La kuweza kutumia?’

11. Wa kwanza nitasema
Bwana Shambi bin Dima
Ndiye makata huruma
Na kinara alipewa.

Mtambaji anasimulia matukio ambayo yeye si mshiriki; yuko kando na anayoyasimulia. Kwa mujibu wa Mohochi (2000) na Mohammed (1995) mtindo wa namna hii wa kusimulia, ambapo msimulizi anaelewa kila kitu kinachotendeka, pamoja na wale wanaotenda unajulikana kama usimulizi maizi au usimulizi wa mwakote. Msimulizi anazijua siri zote za wahusika na anaweza kuwa kila mahali. Katika beti za 12 na 13, msimulizi anatueleza sifa za Binti Hanifu kama ‘asiye na hofu wala shaka.’ Kisha anatufahamisha kuwa ana sifa nyingine ambazo anatueleza baadaye. Msimulizi maizi ana uhuru wa kuamua ni yapi atakayosimulia na yapi atakayoacha nje ya usimuliaji wake. Kwa mfano, katika beti za 89 na 90, anasema:

<p>89. Hayo aliyetamka Sitaweza kuandika Beti kumi zitafika Ndipo yapate timia.</p>	<p>90. Kwanza hayo ni matusi Yafaa kuyakorosi Si (h)aribu karatasi Kwa neno lisilo njia.</p>
---	--

Katika beti hizi msimulizi ameamua kutoeleza maneno aliyoyatamka Bwana Shambi kwa sababu hayaoneshi heshima. Kulingana na msimulizi, kinara wa wachawi alitamka maneno ya aibu yasiyofaa kusimuliwa. Kwa kufanya hili, msimulizi anatuelekeza katika

mkondo maalumu wa mawazo anaoupendelea. Anatumfanya tuwe na mwelekeo fulani kuhusu Bwana Shambi.

Msimulizi maizi anayejitokeza katika utenzi huu ametamba kote kule ambako hadithi inatukia, akiyaweka wazi matukio yote. Anatutoa kijijini Panenene (ubeti 4), mpaka mahali pa siri walipokuwa wakikutana wachawi (ubeti 41); msituni ambapo Salima anavutwa kwa uchawi na kutendewa unyama (ubeti 78); kijijini tena kwa Salima ambapo msako unafanywa (ubeti 133); mjini Ruvuja ambapo ripoti inapelekwa (ubeti 197); kijijini ambapo maiti inagunduliwa (ubeti 239) na polisi kuitwa kupeleleza na kutiwa mbaroni kwa washukiwa (beti 277, 288). Anatupeleka Mteniyapa ambapo wazee wanaandika barua kuomba washukiwa waachiliwe ili washughulikiwe na Nguvumali (ubeti 299) kisha msimulizi anatusimulia jinsi Nguvumali alivyofanya uganga wake na kuwakabidhi kwa polisi (beti 350-351). Baadaye, Nguvumali na wawakilishi wa serikali wanazunguka miji kulisha watu uganga katika juhudi za kuisafisha dhidi ya urogi (ubeti 355). Mwisho anatupeleka mahakamani walipohukumiwa na hata kifungoni walikofungwa wachawi (beti 377-380).

Msimulizi-maizi wa nafsi ya tatu wakati mwingine anaingia katika nafsi na akili za wahusika na kutueleza yaliyomo. Kwa mfano, katika (beti 210-222) ndoto ya Bwana Shambi ambayo inabashiri yatakayotokea baadaye Nguvumali alipofika inasimuliwa. Msimulizi ameingia katika nafsi ya mhusika na kutueleza yale aliyoyaona katika ndoto. Waarabu na Waswahili walifika kijijini kujionea uganga wa Nguvumali. Aidha, tunaalezwa (ubeti 312) kuwa baiskeli zilijaa mahali pale kama alivyokuwa ameona Bwana Shambi katika ndoto. Baadaye alianza kudondokwa na makamasi, akaona kizunguzungu na kushindwa kusimama (beti 321, 341); ikabidi abebwe kwa machela kupelekwa nyumbani alikotoa vyombo vya kichawi alivyokuwa akitumia kuwadhuru watu.

Aidha, katika beti nyingi msimulizi horomo amejitokeza. Kwa mujibu wa Mbatia (2001), msimulizi horomo hutoa maelezo tu bila kuingilia hadithi au kuhusika ili kutoa ufafanuzi au kudokeza msimamo wake. Katika beti zifuatazo, msimulizi anatupeleka tu yale yaliyotendeka baada ya maiti ya Salima kupatikana (beti 272-273):

<p>272. Usiku wa ufajiri Ikaja mvua ya kweli Hapana kujistiri Walapo kukimbilia.</p>	<p>273. Killa mtu anajuta Adhabu wanayopata Ndoto walizoota Dalili inatokea.</p>
--	--

Kiwango kingine cha msimulizi wa nafsi ya tatu (horomo) kinabainika pale ambapo mtunzi anawaacha wahusika kuzungumza au kusemezana baina yao bila kuwaingilia. Kwa njia hiyo, wanaendeleza usimulizi wa hadithi. Kwa mfano, yafuatayo ni mazungumzo baina ya wachawi:

16 ‘Sikilizeni nisemayo

Tena make kitako

Tufanye mji zinguo

Miaka imetimia

Majibizano haya yanaendelea hadi ubeti wa 24. Beti nyingine ambapo wahusika wanaendeleza usimulizi kwa majibizano ni 27- 30 na 32- 34. Katika beti za 45 - 56, ni majibizano baina ya Binti Jizi, Binti Ramadhani na Binti Hanifu. Beti za 61- 65 ni majibizano baina ya Binti Ramadhani na Bwana Shambi, katika beti za 80 - 83 ni maneno ya Binti Hanifu, dadake Salima anapomkabidhi dadake kwa wachawi ili wamtoe kafara. Katika beti za 102 - 113, Salima anazungumzia wachawi hasa dadake Binti Hanifu. Beti za 114-123, Binti Ramadhani anaendeleza usimulizi; anajaribu kuwarai wenzake wamwachilie Salima. Mazungumzo ya aina hii yanapatikana kwa wingi katika utenzi huu. Usimulizi ukiendelezwa na majibizano ya wahusika nafsi ya kwanza inatumika.

Mbali na majibizano ya wahusika, tunapata mkabala wa msimulizi penyezi. Huyu kulingana na Mbatia (2001) na Wamitila (2003), hutoa maoni au hufafanua matendo ya wahusika na matukio ya hadithini au hata kutoa mapendekezo. Mathalani ubeti wa 186 msimulizi anasema:

186. Yale aliyoeleza

Anafanya ninatengeneza

Kumbe khadithi ya pweza

Makaa kujiparia.

Katika ubeti huu, msimulizi anatoa tathmini yake kuhusu tendo la Bwana Shambi la kupendekeza mganga Nguvumali aalikwe Panenene ili asaidie katika uchunguzi wa mauaji ya Salima. Kwa maoni ya msimulizi-mtunzi, kitendo cha Bwana Shambi kilikuwa sawa na kujiongezea shida. Mtunzi anatumia kuwa Bwana Shambi

alipopendekeza Nguvumali aalikwe, alifikiria anatengeneza mambo (mshororo wa 2) lakini Nguvumali alipofika alimfanya yeye (Bwana Shambi) kuaibika kwa kukiri hadharani kuwa amehusika katika mauaji ya Salima. Aidha, katika beti 333-385 alitoa vyombo vya kichawi, vilivyomfanya ashtakiwe na kufungwa miezi tisa gerezani (ubeti 378). Msimulizi amekitathmini kitendo cha Bwana Shambi na kutoa maoni yake. Anamlinganisha Bwana Shambi na pweza anayejipalia makaa.

Katika kutamatisha sehemu hii, imebainika wazi kuwa, *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* umewasilishwa kwa njia kadhaa lakini njia kuu ikiwa ni usimulizi. Matukio na wahusika yamewasilishwa kwa kuelezwa au kusimuliwa na msimulizi ambaye amejibainisha wazi kama mtunzi. Amesimulia kwa kuchanganya usimulizi wa nafsi ya kwanza na ya tatu. Amesimulia matukio ambayo yeye si mshiriki lakini ameyashuhudia yakitendeka. Aidha, katika sehemu nyingine amewaachia wahusika kupitia usemezano au majibizano yao kuendeleza usimulizi wa hadithi. Hili limewafanya wajitokeze kwa njia iliyo wazi.

7.0 Hitimisho

Kutokana na utafiti wetu uliochunguza fani ya usimulizi, imebainika kuwa usimulizi ni mtindo wa uwasilishaji. Mtindo huu unatumika katika kazi za kifasihi, ikiwemo tenzi. Kila kazi huwa na hadithi au ujumbe ambao sharti umfikie msomaji au hadhira yake kupitia kwa msimulizi. Msimulizi anaweza kubainika na kutambuliwa moja kwa moja au ikawa hajidhihirishi wala kutambuliwa kwa urahisi. Katika utenzi huu msimulizi amejibainisha kama mtunzi. Pia, imebainika kwamba *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* una hadithi iliyo na msuko wa moja kwa moja. Tunapata matukio yanayojenga vitushi kama vile kukutana kwa wachawi kisiri na kuamua kutekeleza njama ya kutoa kafara ya binadamu; kisha mwathiriwa ambaye ni dada wa mmoja wa wachawi anapotea na baadaye kupatikana akiwa ameuawa. Wanakijiji wanatoa habari kwa serikali na pia kumwita mganga maarufu wa jadi ili awasaidie kukitegua kitendawili cha kupotea na kupatikana kwa mwathiriwa akiwa ameuawa na kukatwa ulimi, jambo wanalolihusisha na uchawi.

Uchunguzi huu umebainisha kuwa hadithi hii imesimuliwa kwa aina mbili kuu za usimulizi: usimulizi wa nafsi ya kwanza na wa nafsi ya tatu. Usimulizi wa nafsi ya tatu ndio umetawala sehemu kubwa ya utenzi huu japo umekatizwa hapa na pale na usimulizi wa nafsi ya kwanza; aidha wa wahusika au mtunzi-msimulizi. Viwango mbalimbali vya msimulizi wa nafsi ya tatu vimejitokeza; msimulizi-maizi, horomo na penyezi. Wakala wa usimulizi ni mtunzi anayesimulia aliyoyashuhudia yakitendeka. Hata hivyo, katika baadhi ya sehemu za utenzi huu, imebainika kuwa, wahusika wenyewe katika majibizano

yao, wameendeleza usimulizi na kuweza kujibainisha kwa njia iliyo wazi zaidi. Uchangamani huu wa mitindo ya usimulizi umemwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa msomaji bila kumkinaisha na kumchosha kwa mtindo mmoja.

Marejeo

- Allen J .T .W. (1971). *Tendi. Six Examples of Kiswahili Classical Verse*. Nairobi: Heinman Educational Books Ltd.
- Aristotle – “Poetics” (350 Kabla ya kuzaliwa kristo. Tafsiri ya S.H. Butcher, 1994-2009)
- Baldick, G. (1990). *The Concise Oxford Dictionary of Literacy Terms*. New York: Oxford University Press.
- Burundi, R.N. (2011). ‘Usimulizi katika *Utenzi wa Swifa wa Nguvumali*’. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuka.
- Chiraghdin, S. & Mnyapala, M. (1978). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Gerald, A. (1981). *African Languages Literature. An Introduction to the Literary History of Sub-Saharan Africa*. Burnt Hill: Longman Group Ltd.
- Gibbe, A. G. (1994). *Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia*. Tasnifu ya Uzamifu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi.
- Ismail, bin Hassan. (1968). *The Medicine Man: Swifa ya Nguvumali*. (ed.) Lienhardt Oxford: Clarendon Press.
- Kanar, C. (2001). *The Confident Writer*. New York: Houghton Mafin Company.
- Karama, M. R. (1996). *Al- Inkishafi: Ushahidi wa Usemezo katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Heinman.
- Lienhardt, P. (Mh.) (1968). Hassan bin Ismail, *The Medicine Man. Swifa ya Nguvumali*. Oxford: Clarendon Press.
- Masinde, E. W. (2002). *Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui*. Tasnifu ya Uzamifu (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mazrui, A. M. & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publisher.
- Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishers.
- Mlamali, M. (Mh.) (1973). *Inkishafi*. Nairobi: Longman.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nadhari ya Kiswahili*. Nairobi: East Africa Educational Publisher.
- Mohochi, E. S. (2000). Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini. Katika *Nordic Journal of African Studies* 9(2): uk.49-59.
- Momanyi, C. (1991). *Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al-Inkishafi*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Momanyi, C. (1998). *Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika Jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamifu (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publisher.
- Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziyya*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mukuthuria, M. (2007). 'Upekee wa Utenzi wa Swifa ya Nguvumali: Utenzi wa Mpito, Mseto wa Imani za Jadi na Usasa'. Katika *Nordic Journal of African Studies* 16 (3) uk. 298 - 319.
- Mulokozi, M.M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nyanchama, M. B. (2004). 'Matumizi ya Taswira na Ishara katika Sauti ya Dhiki'. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

